TANGAZO LA SERIKALI Na 279 la Tarehe 29/06/2018

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA 290)**

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA MJI WA BABATI ZA MWAKA 2018

*Jina na tarehe ya kuanza kutumika*

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Babati za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

*Eneo la matumizi*

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Babati.

*Tafsiri*

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Babati;

"Madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, kokoto, na mawe yanayochimbwa katika eneo la Halmashauri;

"Maeneo yasiyoidhinishwa" maana yake ni maeneo ya mito, madaraja, barabara, mashamba ya watu, mijini

pamoja na maeneo mengine yanayofanana na hayo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*Sura 290*

"Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa na mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi;

"Wakala" maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni, taasisi, asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.

*Ukaguzi*

4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayekusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba anatoa taarifa kwa Halmashauri ili eneo hilo likaguliwe kuhakikisha kwamba uchimbaji huo hautaenda kinyume na Sheria za Mazingira.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukubali au kukataa eneo lolote kuwa au kutokuwa eneo la machimbo ya madini ya ujenzi.

*Kibali cha uchimbaji*

5.(1) Mtu yeyote anayetaka kuchimba madini katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuomba na kupata kibali cha kuchimba madini kutoka Halmashauri.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitaeleza aina ya madini yanayochimbwa na eneo litakalochimbwa madini hayo. Kibali kinachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitalipiwa Ada ya shilingi laki mbili kwa mwaka.

(3) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga machimbo yoyote ya madini ya ujenzi kama itaona kufanya hivyo ni kwa maslahi ya Halmashauri na umma kwa ujumla.

*Ushuru*

6. (1) Mtu yeyote atakayesafirisha madini ya ujenzi kutoka eneo yalikochimbwa kwenda maeneo mengine atalipa ushuru kwa tripu kwa viwango vilivyooneshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru huo utatozwa mara baada ya msafirishaji kununua madini kutoka kwa mchimbaji au kupakia madini hayo katika chombo ambacho atakitumia kwa ajili ya kusafirishia.

(3) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo na barabara zinazoelekea au kutoka maeneo ya machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

(4) Mnunuzi yeyote atakayeshindwa kulipa ushuru anaotakiwa kulipa atatakiwa kupakua madini ya ujenzi kutoka katika chombo au kutochukua madini hayo mpaka hapo atakapolipa ushuru anaodaiwa.

*Wajibu wa kulipa ushuru*

7. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ushuru kulipa ushuru huo kama ilivyoelekezwa katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo kumzuia dereva au gari lolote kujishughulisha na usafirishaji wa madini ya ujenzi ikithibitika kwamba kuna ukiukwaji au uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi.

*Ushuru kulipwa kwa Halmashauri*

8. (1) Ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa kwa Halmashauri au wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha malipo hayo.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu aliyelipa ushuru kudai risiti na hautakuwa utetezi kwa mtu yeyote kudai kuwa amelipa ushuru lakini hakupewa risiti.

*Kufunika magari*

9. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari au magari yanayobeba madini ya ujenzi kuhakikisha kwamba gari au magari yake yamefunikwa ili kuzuia uharibifu na

uchafuzi wa Mazingira.

*Muda wa machimbo kuwa wazi*

10. Maeneo yote ya machimbo ya madini yatafunguliwa kuanzia saa kumi mbili alfajiri (12:00) na kufungwa saa kumi na mbili jioni (12:00).

*Vituo vya ukaguzi*

11. (1) Halmashauri itaanzisha vituo kwa ajili ya ukaguzi wa magari yanayobeba madini ya ujenzi katika barabara zinazoingia na kutoka machimboni.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila dereva kusimama katika kituo cha ukaguzi wa madini na kuonyesha stakabadhi aliyolipia ushuru na endapo hatakuwa na stakabadhi hiyo atatakiwa kulipa ushuru kwa viwango vilivyoainishwa na Sheria Ndogo hizi.

*Halmashauri kutowajibika kwa hasara*

12. Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi wakati wa kukusanya ushuru isipokuwa kama hasara hiyo itatokana na uzembe wa Halmashauri.

*Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa*

13. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote yanapochimbwa madini ya ujenzi kwa ajili ya kukagua na kukusanya ushuru.

*Makosa*

14. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote chini ya Sheria Ndogo hizi endapo:-

(a) atakataa au kushindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Mwidhiniwa;

(b) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(c) atakataa au kujaribu kukataa kulipa ushuru;

(d) atashawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru;

(e) atakwepa au atajaribu kukwepa kulipa ushuru;

(f) atachimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyoidhinishwa;

(g) atachimba shimo kubwa kwa ajili ya madini ya ujenzi na kuliacha bila kufukia au kupanda miti au mimea mara baada ya madini hayo kuisha;

(h) atachimba madini katika eneo lisiloruhusiwa hasa maeneo ya barabara na maeneo ya hifadhi.

*Adhabu*

15. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Kufifilisha kosa*

16. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama iliyoelekezwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

**JEDWALI LA KWANZA**

*Limetungwa chini ya kifungu cha 6 (1)*

| NA. | AINA YA MADINI | KIASI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mawe,Mchanga,Kokoto,Kifusi,Changarawe, Chokaa na udongo. | 5,000/= | Lori la tani 1-7 kwa Tripu. |
| 2. | Mawe,Mchanga,Kokoto,Kifusi,Changarawe, Chokaa na udongo | 10,000/= | Lori la tani 8-zaidi kwa Tripu. |

**JEDWALI LA PILI**

**FOMU YA KUFIFILISHA KOSA**

(*Limetungwa chini ya kifungu cha 16)*

Mimi ........................................................ wa SLP..................... ninayefanya biashara ya ........................................................ katika eneo la ...................................... lililopo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Babati. nakiri kuwa leo tarehe ...................... nilikiuka kifungu cha .................. cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Babati za mwaka 2018. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ..........................................................

Jina ............................................................

Mbele yangu.................................................

Saini ....................................................

Wadhifa ...........................................

Nembo na Muhuri wa Halmashauri ya Mji wa Babati umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani ulioitishwa tarehe 16 Mwezi Novemba Mwaka 2017 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na:-

FORTUNATUS H. FWEMA
*Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Mji wa Babati*

L.S

KIBIKI MOHAMED KIBIKI
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji wa Babati*

NAKUBALI,

Dodoma
07/06/2018

SELEMANI S. JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi – OR-TAMISEMI*